**MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA UONGOZI NA MIPANGO CHA MWEZI NOVEMBA CHA TAREHE 21/12/2021.**

**A: WAJUMBE WALIOHUDHURIA**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe.Methew Mbaruku | D/Magamba | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe.Hatibu Ulanga | D/Mbaramo | Mjumbe |
| 3. | Mhe. Jambia Shehoza | D/Mn'garo | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Mariane Werongo | D/V/Maalum | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Yasini Billa | D/Lunguza | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Catherine Shemdoe | D/V/Maalum | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Marieta Msagati | D/V/Maalum | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Ahamadi Ngoma | D/Dule M | Mjumbe |
| 9. | Ikupa Mwasyoge | Mkurugenzi Mtendaji | Katibu |

**B: WAJUMBE WALISIOHUDHURIA.**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe.Shabani Shekilindi | Mbunge Lushoto | Kwa taarifa |
| 2. | Mhe. Rashidi A. Shangazi | Mbunge Mlalo | Kwa taarifa |
| 3. | Mhe. Iddi Kipande | Diwani/K/Kwai | Kwa Taarifa |

**C: WAKUU WA IDARA**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Nice Ngasala | Afisa Utumishi |
| 2. | Said Nguzo | Kny. Mkaguzi wa Ndani |
| 3. | Petronila Benedict | Kaimu Mhandisi wa Ujenzi |
| 4. | Athumani Hazali | Afisa Utawala Bora |
| 5. | Ayubu Omari | Afisa Kilimo na Umwagiliaji (W) |
| 6. | Justin Njuu | Afisa Mipango (W) |
| 7. | Joyce Mramba | Afisa Maendeleo ya jamii |
| 8. | William Chawala | Kaimu Mweka Hazina (W) |
| 9. | Simon Mgonja | Kaimu Afisa Elimu Msingi (W) |
| 10. | Godfrey Andrew | Mganga Mkuu (W) |
| 11. | Thomas Lyimo | Kaimu Afisa Mazingira |
| 12. | Tunu Bushiri | Kaimu Afisa Ugavi (W) |
| 13. | Emanueli Ebenezer | Afisa Elimu Sekondari |
| 14. | Eliezer Moses | Afisa Mifugo na Uvuvi |
| 15. | Neema Mafie | Afisas Mapato |
| 16. | Arcadius Ndunguru | Afisa Nyuki |
| 17. | Salmin Mziray | Kny.Afisa Ardhi na Maliasili |
| 18. | Menrad Mvimbile | Afisa TEHAMA |
| 19. | Godfrey Mwakafwila | Afisa Biashara |
| 20. | Godchance Makyao | Kny Katibu Tawala Wilaya |
| 21. | David Masanyika | TEO |
| 22. | Esuvat Kivuyo | Mratibu wa UKIMWI |

**D: SEKRETARIETI**

1. Oscar Ndosi — Mwandishi wa Vikao

Katibu.................................. MKURUGENZI MTENDAJI



Mwenyekiti.................................. MWENYEKITI HALMASHAURI YA WILAYA LUSHOTO

**AGENDA NA 121/12/2021/2022. KUFUNGUA KIKAO**
Katibu aliwasalimu wajumbe na kuwakaribisha katika kikao hicho Alimkaribisha mwenyekiti kufungua kikao, Mwenyekiti alitamka kufungua Kikao saa 4:27 Asubuhi.

❖ **KUTHIBITISHA AGENDA**

Jumla ya agenda 12 ziliwasilishwa mbele ya wajumbe na kuthibitishwa ili ziweze kujadiliwa katika kikao hicho.

**AGENDA NA. 122/12/2021/2022:- KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA FEDHA UONGOZI NA MIPANGO CHA TAREHE 21/12/2021.** Mwandishi wa vikao aliomba ridhaa ya Mwenyekiti kusoma au kutosoma muhtasari huo. Kwa kuwa wajumbe walishasoma muhtasari wa kikao kilichopita, Mwenyekiti aliwaongoza kupitia ukurasa mmoja baada ya mwingine ili kufanya masahihisho ya kimantiki na kiuchapaji. Baada ya wajumbe kuridhia kilichoandikwa ni sahihi, Katibu na Mwenyekiti walisaini muhtasari huo kuwa kumbukumbu halali ya Halmashauri ya Wilaya Lushoto.

**AGENDA NA. 123/12/2021/2022:- KUPITIA UTEKELEZAJI WA YATOKANAYO NA KIKAO CHA TAREHE 21/12/2021**

1. Mazao yaliyovunwa kuanzia July hadi Octoba 2021 katika Halmashauri ya Lushoto yawasilishwe.Taarifa kabla haijatumwa Halmashauri ipite kwenye WDC.

**UTEKELEZAJI:-** Taarifa sahihi zinaendelea kukusanywa kutoka kwenye kata,Tunaomba taarifa hii iwasilishwe kikao kijacho.

2. Taarifa ya mapato ya mwezi Octoba na Novemba 2021 kutoka kwenye kata yaweze kuwasilishwa kikao kijacho.

**UTEKELEZAJI:-** Taarifa iliwasilishwa ikionesha jumla ya mapato kutoka kwenye kata kwa mwezi Octoba ni TZS 8,829,500.00 na kwa mwezi Novemba ni TZS 9,543,600.00 kata za Mbwei,Malibwi,Mbaramo,Kilole,Ngulwi,Shaghayu na Ngwelo hawakuwa na mapato yoyote waliokusanya.

3. Taarifa ya madeni Halmashauri inayodai na inayodaiwa iwasilishwe kikao kijacho.

**UTEKELEZAJI:-** Kiasi tunachodai ni TZS 503,381,722,na tunachodaiwa ni TZS 2,834,128,955.23,

4. Mapato ya nyumba za kulala wageni kuanzia July hadi November 2021 yawasilishwe kikao kijacho.

**UTEKELEZAJI:-** Mapato yaliyopatikana July hadi Novemba kwenye nyumba za kulala wageni ni TZS 3,888,350.

5. Mzabuni yoyote anaesafirisha madini ya ujenzi asilipwe fedha zake hadi awe amekatwa ushuru wa Halmashauri.Orodha ya wazabuni walioanza kukatwa ushuru wa Halmashauri iwasilishwe.

**UTEKELEZAJI:-** Baadhi ya wazabuni waliolipa ushuru wa madini ya ujenzi ni pamoja na Frank Olotu mchanga tripu 50 amelipa 150,000,Gervas Kavishe kokoto tripu 20 amelipa 60,000,Mdoe Sangoda mawe tripu 80 amelipa tripu 80 na Fadhili Juma mawe tripu 36 na mchanga tripu 22 amelipa 174,000.

6. Idadi ya Bar kwa kila kata iwasilishwe kikao kijacho.

**UTEKELEZAJI:-** Barua yenye Kumb.Na/M.10/25/vol iii/186 ya tarehe 13/12/2021 imeandikwa kwa watendaji wa kata kuweza kuwasilisha taarifa hizo.

Katibu..................  Mwenyekiti..................

MWENYEKITI

Ndugu Sebarua Shemboza aweze kuitwa na kutaarifiwa kuwa vibanda vitavunjwa lakini ataingia mkataba wa miaka 5 na Halmashauri wa kujenga kwenye ardhi ya Halmashauri, na miaka miwili imepita tangu vibanda vijengwe,mkataba huo utakuwa umebakisha miaka 3,na atapashwa kulipa gharama ya miaka 2 ya nyuma Halmashauri.

**UTEKELEZAJI:-** Ndugu Sebarua Shemboza ameitwa na amefika,ameridhia kulipa na kujaza mkataba.

8. Kikao cha wakuu wa idara kichambue na kuweka utaratibu wa kutoza ushuru wa bodaboda kwa Halmashauri nzima.

**UTEKELEZAJI:-** Kwasasa kunafanyika maandalizi ya kuwa na sheria ndogo ili kuweza kukusanya ushuru huu kwa kuzingatia sheria na taratibu.

9. Fundi aliyejenga soko la Hambalawei aweze kutafutwa kuja kumalizia kazi pamoja na mapendekezo ya mkaguzi kufanyiwa kazi.

**UTEKELEZAJI:-** Barua yenye KUMB.NA/LDC/AD/PF/1086/196 ya tarehe 13/12/2021 imeandikwa kwa mtendaji wa kata ya Shume kumtafuta fundi alikuwa anajenga soko aje kumalizia ujenzi na jamba hili lifanyike kwa haraka.

10. Mh Diwani Kata ya Lunguza pamoja na mkaguzi wa ndani wawasilishe taarifa za maandishi kuhusu cement zilizoganda kata ya Lunguza.

**UTEKELEZAJI;-** Mh diwani alitoa taarifa kuwa mifuko hiyo ilitumika katika shughuli nyingine katika kata ya Lunguza na kuagizwa na kikao kwenda kuleta Mihutasari iliyoelekeza matumizi ya mifuko hiyo.

11. Mkaguzi wa ndani afuatilie Zahanati ya Mtae kwanini wanachukua fedha bila kuwa na kitabu cha kukusanyia mapato tangu mwezi Septemba 2021.

**UTEKELEZAJI:-** Zahanati ya Mtae katika kipindi cha mwezi Septemba 2021 imekusanya jumla ya TZS 114,000 kutoka kwa wateja 19 hata hivyo hawakuwa na vitabu vya kukusanyia kwa matarajio ya kufungiwa mfumo ambao hata hivyo haujafungwa kutokana na manunuzi ya vifaa kutokamilika.

**12.** Wanachi waliojenga kwenye eneo la wazi Sinza na hawalipi pango la ardhi Halmashauri waandikiwe notice ya kubomoa majengo yao.Kikao kijacho taarifa iwasilishwe utekelezaji umefikia wapi.

**UTEKELEZAJI;-** Wananchi wawili waliobaki mmoja amekiri kuanza kulipa kodi ya pango la ardhi Halmashauri,mwananchi mmoja aliyebaki amepewa notice ya kuvunja jengo lake.

**13.** Mapato ya viwanja Mnazi kwa mwezi Novemba 2021 yaweze kuwasilishwa.

**UTEKELEZAJI:-** Kwa mwezi Novemba 2021 fedha iliyokusanywa ni TZS 2,015, 100.

**AGENDA NA. 124/12/2021/2022:- TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWEZI NOVEMBA 2021.** Ofisi ya Mweka Hazina (W) iliwasilisha kikaoni taarifa ya mapato na matumizi kwa mwezi Novemba 2021 kama ifuatavyo:-

**A: MAPATO**

Katika kipindi cha mwaka wa fedha **2021/2022** Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto ilikisia kukusanya jumla ya **Tshs. 42,967,982,711.00** kutoka vyanzo mbalimbali vya mapato, ikijumlishwa pamoja na bakaa ya **Tshs.**

Mwenyekiti............ MWENYEKITI HALMASHAURI YA WILAYA LUSHOTO



Katibu.............. MTENDAJI

**36,518,590.00** kutoka mwaka wa fedha **2020/2021** inafanya bajeti ya mapato yote kwa mwaka kufikia jumla ya **Tshs. 43,004,501,301.00.**

**MAKUSANYO YA MAPATO**

Katika kipindi cha **Julai 2021 hadi Novemba 2021,** Halmashauri imekusanya jumla ya **TZS. 18,240,990,302.00** kutoka katika vyanzo vyote vya mapato sawa na asilimia **42:21%** ya makisio kwa mchanganuo ufuatao;-

a) Mapato ya vyanzo vya ndani ni **Tshs. 895,908,068.00** sawa na asilimia **36.40%.**
b) Ruzuku kwa idara za utawala(GPG) ni **Tshs. 00.00** ni sawa na **00.00%**
c) Ruzuku ya Matumizi ya kawaida ni **Tshs. 552,934,582.00** ni sawa na asilimia **43.37.**
d) Mishahara ni **Tshs.12,384,049,000.00** ni sawa na asilimia **42.01%**
e) Miradi ya Maendeleo ni Tshs. **4,408,098,652.00** ni sawa na asilimia **44.49%**

**B:MATUMIZI**

Vilevile katika kipindi cha mwezi **Julai 2021-Novemba 2021** mwaka wa Fedha **2021/2022,** Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto katika kutekeleza majukumu yake mbalimbali imetumia Jumla ya **Tshs. 18,240,990,302.00** sawa na asilimia **42.21%** ya makisio yaliyopangwa kwa mwaka, ambapo:

a) Matumizi katika Maeneo ya Idara za Utawala ni Tshs. **1,227,021,561.00** ni sawa na Asilimia **33.90%**
b) Matumizi katika maeneo yanayopata Ruzuku za kawaida ni Tshs.**261,978,258.00** sawa na asilimia **34.17%**
c) Matumizi kwa ajili ya Mishahara ni Tshs. **11,596,962,500.00** sawa na asilimia **37.44%**
d) Matumizi katika maeneo ya Miradi ya Maendeleo ni Tshs. **4,408,098,652.00** sawa na asilimia **44.49%**

Baada ya taarifa hiyo kuwasilishwa, wajumbe waliipokea, kujadili na kushauri yafuatayo;-

- Ripoti ya mapato na matumizi kwa mwezi Novemba 2021 ilirudishwa na kuagizwa ziletwe sababu kwanini mapato kwa mwezi Octoba na Novemba 2021 yameshuka kwa zaidi ya milioni 100.

**AGENDA NA. 125/12/2021/2022:- TAARIFA YA KITENGO CHA UTAWALA BORA KWA MWEZI NOVEMBA 2021.** Ofisi ya Utawala bora iliwasilisha taarifa yake kwa kipindi cha mwezi Novemba 2021 kama ifuatavyo:-

**A. Mihtasari.**

I. Mihtasari ya Halmashauri za vijiji imewasilishwa 78/125 kwa mwezi Novemba 2021 sawa na asilimia 62.

II. Mihtasari ya mikutano mikuu ya vijiji kwa mwezi Novemba 2021 imewasilishwa 70/125 sawa na asilimia 56

III. Mihtasari ya kamati za Maendeleo ya kata imewasilishwa 30/33 sawa na asilimia 90.

Katibu....................  Mwenyekiti.........................

MKURUGENZI MTENDAJI (W) LUSHOTO

MWENYEKITI HALMASHAURI YA WILAYA LUSHOTO

IV. Mihtasari ya vikao vya Idara na vitengo vya Halmashauri ya Wilaya Lushoto imefanyika 13/14 sawa na asilimia 92.

**Migogoro.**

Hakuna.

Baada ya kuwasilishwa taarifa ilipokelewa, kujadiliwa na kuagizwa yafuatayo;-

- ❖ Taarifa ilitolewa kuwa utekelezaji wa ujenzi wa madarasa ya UVIKO 19 kwa elimu msingi ni 29% na kwa elimu Sekondari ni 65%.
- ❖ Kikao kijacho iletwe taarifa ya miradi ya tozo na uviko imefikia wapi.

**AGENDA NA. 126/12/2021/2022:- TAARIFA YA KESI ZA HALMASHAURI HADI KUFIKIA MWEZI NOVEMBA 2021.**Afisa sheria aliwasilisha taarifa hiyo kama ifuatavyo:- Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto dhidi ya Amina Nguzo kuhusu nyumba iliyopangishwa kinyume na taratibu/sheria zaidi ya miaka 300,maombi ya Reference kwa maamuzi ya Halmashauri kulipa gharama ya kesi TZS 3,270,000 ipo hatua ya kusikilizwa.

Kijiji cha Migambo dhidi KKKT-DKMS la nusu madai ya kuvamia eneo heka lenye thamani ya TZS 6,300,000 ipo hatua ya kusikilizwa.

Yoram Msumari VS Kijiji cha Viti na Salim Selemani mgogoro wa ardhi mamombi ya kukazia hukumu ipo hatua ya kusikilizwa.

Salim Mavale VS Kijiji cha Kireti rufaa ya kupinga maamuzi ya baraza la ardhi na nyumba la Wilaya ipo hatua ya kusikilizwa.

Hashim Saleh Kihahio VS Kijiji cha Mng'aro na MIC (T) LTD madai ya kuvamia eneo la kijiji na kulikodisha kwa kampuni inayomiliki minara ya simu gharama ya kesi 6,000,000 ipo hatua ya kusikilizwa.

Kijiji cha Viti VS Yoram Msumari na Salim Selemani maombi ya kuongezewa muda,kufuta maamuzi ya upande mmoja ipo hatua ya maamuzi madogo.

David Shemakange dhidi ya Alfani Msigiti,Ramadhani Mdimu,Halmashauri ya Lushoto,mgogoro wa ardhi kupinga uhalali wa halmashauri kuuza eneo la kiwanda kwa mlalamikiwa wa kwanza thamani ya kesi ni TZS 16,000,000 ipo hatua ya kusikilizwa.

Usambara Fruit Processing Company LTD VS Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto, madai ya heka 4.39 zilizomegwa na kujengwa shule ya Sekondari Magamba yenye thamani ya TZS 50,000,000 ipo hatua ya kusikilizwa.

Theodory Joseph Kamote and Others VS Kijiji cha Irente,madai ya kuvamiwa eneo la kivutio cha Irente ipo hatua ya kutajwa.

Hadi mwezi Novemba 2021 kesi zilizopo ni 09.

Baada ya kuwasilishwa taarifa ilipokelewa, kujadiliwa na kuagizwa yafuatayo;-

- ❖ Kwenye kesi ya David Shemakange dhidi ya Alfani Msigiti, Ramadhani Mdimu&Halmashauri ya Lushoto ifuatiliwe kama Halmashauri ya Bumbuli wameunganishwa kwenye kesi.

Katibu..................  Mwenyekiti..........

MKURUGENZI MTENDAJI (W) LUSHOTO

MWENYEKITI HALMASHAURI YA WILAYA LUSHOTO

**AGENDA NA. 127/12/2021/2022:- OMBI LA KIBALI CHA UJENZI WA VYUMBA VYA MADARASA, VYOO PAMOJA NA UKARABATI WA MIUNDOMBINU CHAKAVU SHULE YA MSINGI TEWE.** Kata ya Lunguza ilipata msaada tajwa hapo juu kutoka kwa shirika lisilo la kiserikali linaloitwa COMFORT AID INTERNATIONAL lenye makao makuu nchini Marekani na linashirikiana na shirikiana na taasisi mwenyeji ya NYOTA FOUNDATION yenye makao makuu Dar es Salaam,ambapo mashirika haya yanajihusisha na shughuli mbalimbali za kutoa misaada ya huduma za kijamii kama ujenzi wa miundombinu ya elimu,afya na maji.Ambapo wamekubali kufanya yafuatayo katika shule ya msingi Tewe:-

- Kujenga vyumba viwili vya madarasa pamoja na ofisi.
- Watafanya ukarabati wa vyumba vitano vya madarasa vilivyopo sasa.
- Watajenga matundu matano ya vyoo kwa wanafunzi wa kike.
- Watakarabati matundu saba yaliyopo sasa ambayo hayana ubora stahiki kwa wanafunzi.

Baada ya kuwasilishwa taarifa ilipokelewa kujadiliwa na kuruhusiwa kuendelea na ujenzi na ukarabati.

**AGENDA NA. 128/12/2021/2022:- MAOMBI YA ARDHI (ENEO/KIWANJA) KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA LUSHOTO KWA AJILI YA UJENZI WA OFISI NA GHALA LA VIFAA VYA MAAFA.** Tanzania Red Cross Society (TRCS) ni taasisi ya kujitolea huduma za kibinadamu nchini,Kwa mujibu wa kifungu cha 15(2c) cha Sheria ya usimamizi wa maafa(THE DISASTER MANAGEMENT ACT) namba 7 ya mwaka 2015 Tanzania Redcross Society ni mjumbe wa kamati ya usimamizi wa maafa ya kuanzia ngazi ya mkoa,wilaya,kata na vijiji.

TRCS inaleta ombi la kupatiwa eneo/kiwanja kwa ajili ya ujenzi wa ghala na ofisi litakalotumika kuhifadhi vifaa na uratibu wa huduma za kibinadamu katika ngazi ya Halmashauri/Wilaya.

Baada ya kuwasilishwa taarifa ilipokelewa kujadiliwa na kuagizwa kuwa waweze kujibiwa Halmashauri ina viwanja katika kata ya Mnazi na vinauzwa.

**AGENDA NA. 129/12/2021/2022:-MAPOKEZI YA FEDHA KIASI CHA TZS 410,000,000.**

Halmashauri imepokea fedha za ujenzi wa miradi ya afya na elimu kiasi tajwa hapo juu kwa mwezi Desemba 2021 kwa mchanganuo ufuatao:-

| S/N | JINA LA MRADI | KIASI | CHANZO CHA FEDHA |
|---|---|---|---|
| 1 | UJENZI WA MADARASA 6 OFISI ZA WALIMU,MADAWATI NA MATUNDU YA VYOO 24 KWENYE SHULE YA MSINGI HAMBOYO. | 160,000,000 | TEA |
| 2 | UJENZI WA MADARASA 6 OFISI ZA WALIMU,MADAWATI NA MATUNDU YA VYOO 24 KWENYE SHULE YA MSINGI YOGHOI. | 160,000,000 | TEA |
| 3 | UJENZI WA NYUMBA YA MGANGA TATU KWA MOJA ZAHANATI YA KILOLE | 90,000,000 | UVIKO 19 |
| | JUMLA | 410,000,000 | |

Baada ya kuwasilishwa taarifa ilipokelewa kujadiliwa na kupitishwa.

Katibu....................  Mwenyekiti....................

MWENYEKITI
HALMASHAURI YA WILAYA